

TAARIFA YA IDARA YA KILIMO KATA YA NAMATUTWE

1. UTANGULIZI

Kata ya Namatutwe ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, umbali wa kilomita 78 kutoka ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Masasi.

Kata ya Namatutwe ina jumla ya kaya 2,725 na jumla ya watu ni 20,576 ambapo kaya 2,665 zinajishughulisha na kilimo. Eneo la kata ya Namatutwe lina ukubwa wa hekta 42,343.74, eneo linalofaa kwa kilimo ni hekta 31,757.8 na eneo linalotumika kwa sasa ni hekta 26,994.13 ambalo ni sawa na asilimia 85.

2. UZALISHAJI WA KOROSHO NA UFUTA

Mheshimiwa mkuu wa Mkoa, wakulima wa kata ya Namatutwe wanajishughulisha na kilimo cha mazao ya biashara na chakula ambapo mazao makuu ya chakula ni muhogo na mahindi, wakati mazao makuu ya biashara ni ufuta, korosho, mbaazi na choroko. Lakini pia tumekuwa tukiendelea kuwashauri wakulima kuongeza wigo wa kulima mazao mengine ya biashara kama vile alizeti.

Kata ya Namatutwe ina jumla ya mikorosho ipatayo **378,598** ambayo ilitakiwa iwe inatoa Tani **2,668** kwa mwaka kwa wastani wa uzalishaji wa kilo 8 kwa mti kwa ngazi ya mkulima.

Uzalishaji wa korosho na ufuta kwa miaka mitatu mfululizo ni kama ifuatavyo:

Mwaka	Korosho (Tani)	Ufuta (Tani)
2017/2018	750	678
2018/2019	655	668
2019/2020	505	721
2020/2021	819	

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa mwaka 2018/2019 tuliongoza kimkoa kwa kuwa nafasi ya kwanza kwa kuzalisha ufuta, na kwa msimu uliopita wa 2019/2020 tumekuwa wa kwanza kiwilaya, hivyo tumeweza kuchangia katika mapato ya halmashauri kutokana na mazao hayo.

3. KAMPENI ONDOA MAPORI ONGEZA UZALISHAJ

Katika kuhakikisha kampeni hii inatekelezwa na kuleta mafanikio tayari tuna hekta **196** ambazo zitaboreshwa kwa kukata mikorosho iliyozeeka, yenye uzalishaji mdogo, iliyokaribiana sana na kupanda mikorosho sehemu za wazi. Pia baadhi ya wakulima wanaandaa mashamba mapya ili kupanda mikorosho jumla ya hekta 71.4 zimeandaliwa. Hapa tulipo kwenye shamba la mkulima **Bakari Mahamudu Ligaja** ni miongoni mwa wakulima wanaotekeleza kampeni hii.

Aidha tumepokea mbegu ya korosho kilo 83 kutoka Halmashauri na kuzigawa kwa wakulima.

Mheshimiwa mkuu wa mkoa pia katika kutekeleza kampeni tumehamasisha na kuunda kikundi cha vijana cha kuzalisha miche kiitwacho **TUJIFUNZE** na tayari wamezalisha miche 809 ambayo inauzwa kwa wakulima.

4. CHANGAMOTO

- i. Wakulima kutoweka akiba ya fedha kwa ajili ya shughuli za kilimo

Wakulima walio wengi wakishapata fedha wanazitumia zote bila kuweka akiba kwa ajili ya shughuli za kilimo ikiwemo kununua pembejeo.

MWISHO

Mwisho kabisa nitoe shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa kututembelea ili kuona shughuli zinazofanyika katika maeneo yetu. Hii imewapa faraja kubwa sana wakulima na pia itaamsha ari kwa wakulima ya kufanya kazi kwa bidii kwa kuwa imeonesha wazi namna gani serikali inathamini shughuli zinazofanywa na wakulima.

Naomba kuwasilisha.

Siraji M. Suleimani
AFISA KILIMO KATA-NAMATUTWE